

HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA
(BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI MTENDAJI)

MKOA WA RUKWA

SIMU: 025-2802133

FAX: 025-2800301

Email:

ded@sumbawangadc.go.tz



Sanduku la Posta 229
SUMBAWANGA.
TANZANIA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.SDC/A.120/2/243

17/01/2024

TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi ya Mkataba ili kuziba nafasi wazi kama ifuatavyo:-

1. DEREVA - Nafasi 6.

Majukumu ya kazi.

- I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- II. Kuwapeleka Watumishi kwenye maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- III. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
- IV. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- V. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (log Book).
- VI. Kufanya usafi wa gari.
- VII. Kutekeleza majukumu mengine atakayopangiwa na mwajiri.

Sifa za Mwombaji

- I. Awe na cheti cha Kidato cha Nne (IV).
- II. Awe na leseni Daraja C au Daraja E ya uendeshaji magari.
- III. Awe na uzoefu wa kutosha katika uendeshaji wa magari (usiopungua mwaka mmoja) na ambaye hajasababisha ajali.
- IV. Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya uendeshaji wa magari (basic driving course) yanayotolewa na VETA au NIT au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Ngazi ya mshahara.

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Halmashauri.

2. FUNDI SANIFU MSAIDIZI - MECHANICAL (FUNDI MAGARI) - *Nafasi 1.*

Majukumu ya kazi.

- I. Kufanya ukaguzi ili kutambua matatizo ya magari na mitambo na kufanya matengenezo.
- II. Kufanya matengenezo kinga (Preventive maintenance).
- III. Kufanya majaribio ya ubora wa magari na mitambo baada ya matengenezo.

Sifa za mwombaji.

Kuajiriwa wenye elimu ya Kidato cha IV waliofuzu mafunzo ya mwaka mmoja katika fani yenye mwelekeo wa Ufundi Mechanical kutoka VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

Ngazi ya mshahara.

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Halmashauri.

Masharti ya Jumla.

- I. Waombaji wote wawe na umri kuanzia miaka 18 - 45.
- II. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, cheti cha Kidato cha nne na cheti/vyeti vya taaluma ya udereva.
- III. Waombaji waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani nan amba za simu za kuaminika, na majina matatu ya wadhamini.
- IV. Maombi yaambatishwe na picha moja (passport size 1) ya hivi karibuni na iandikwe majina kwa nyuma.
- V. Waombaji wote waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA). Waombaji wasio na Kitambulisho cha Taifa (NIDA) waandike namba ya NIDA kwenye maelezo binafsi (CV).

Maombi yote yatumwe kwa njia ya POSTA kupitia anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga,
S.L.P 229,
SUMBAWANGA.

NB: *Maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya mkono hayatafanyikiwa kazi.*

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/01/2024.


Lightness Stanley Msemu
Mkurugenzi Mtendaji (W)
SUMBAWANGA.

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
SUMBAWANGA**